

**MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA NANE WA WADAU WA KAHAWA
ULIYOFANYIKA KATIKA HOTELI YA NASHERA MOROGORO
TAREHE 18 – 19 MEI 2017**

Na.	Azimio	Mhusika
1.	Tathmini ya mkakati wa maendeleo ya kahawa itengenezewe mpango wa utekelezaji utakaonesha majukumu ya kila mdau na muda wa utekelezaji wake. Sambamba na hilo Kanda zote zinazolima kahawa nchini zifanye vikao vya kupitia tathmini ya nusu mwaka ya utekelezaji wa mpango mkakati wa kahawa ili kufanya mabadiliko.	TCB, LGAs, TaCRI, TCA, TCDF
2.	TaCRI kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ikamilishe upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya utafiti wa kahawa katika Wilaya ya Tarime-Mara na Buhigwe-Kigoma.	TaCRI, LGAs
3.	Wadau wanashauri kwamba TaCRI iwezeshe zaidi kifedha ili iweze kutekeleza majukumu ya utafiti kwa ufanisi.	TCB, WKMU, TCDF, TaCRI
4.	Serikali iendee kutoa ruzuku kwenye zao la kahawa katika uzalishaji wa miche na pembejeo kama mazao mengine ya biashara.	WKMU
5.	Taasisi zinazonufaika na michango ya wadau (TaCRI/Mfuko na Bodi) zitayarisha na zipeleke bajeti yake Serikalini kupitia Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kugharamiwa.	TaCRI, WKMU TCB, TCDF
6.	Kuwepo na mkakati wa kuhamasisha unywaji wa kahawa wa ndani ili kuimarisha bei ya kahawa.	TCB, TCDF, LGAs, TCA, TAWOCA
7.	Mfumo wa usimamizi wa soko la ndani uimarishwe ili kuwezesha uwepo wa bei nzuri kwa mkulima na kuepusha uuzwaji wa kahawa usio rasmi.	TCB, LGAs, TCA
8.	Utafiti wa kina ufanyike kuhakiki uwiano wa kahawa ya matunda kwa kahawa kavu (parchment).	TaCRI, TCB, LGAs,
9.	Halmashauri za Wilaya ziwe na mikakati ya kubadilisha mibuni ya zamani ya kahawa na kupanda miche mipya ya kahawa.	TCB, TaCRI, LGAs
10.	Mkutano wa wadau umeidhinisha matumizi ya shilingi za Kitanzania 200,000,000/- za Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa Tanzania kwa ajili ya kutoa ruzuku ya miche ya kahawa kwa mwaka 2017/2018.	TCDF, TCB, TaCRI
11.	Bodi ya kahawa ishirikiane na Halmashauri za Wilaya kuhakiki takwimu za uzalishaji ili kuboresha zoezi la ukusanyaji wa mapato na uendelezaji wa zao.	TCB, LGAs
12.	Menejiment ya TaCRI ishughulikie madai ya kuwepo kwa wajumbe wasio na sifa ambao wanawakilisha vyama vya ushirika katika Bodi ya TaCRI.	TaCRI
13.	Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ishughulikie changamoto za vyama vya ushirika kwa lengo la kuviimarisha na kuviwezesha kushiriki kikamilifu katika masoko ya kahawa.	WKMU, TCDC

14.	Kuwepo na mipango mahsusi ya kuimarisha ugani ili kuhakikisha zao la kahawa linahudumiwa kikamilifu.	WKMU, LGAs, TaCRI
15.	Bodi ya Kahawa ifanye utafiti na kutoa mrejesho kwa wadau wa jinsi ya kuanzisha mnada kwenye maeneo yanayozalisha kahawa.	TCB
16.	Serikali kupitia Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi itimize ahadi yake ya kuchangia shilingi za Kitanzania bilioni mbili kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa ambayo haijatekelezwa tangu mwaka 2011.	WKMU, TCDF, TCB